“Hili Nalifahamu”
(“This I Know”)

NA

Ellis P. Forsman

“Hili Nalifahamu”

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

“Hili Nalifahamu”

1 Wafalme 17:24

1 Wafalme 17: 24, *“Naye mfalme wa Ashuru akaleta wa kutoka Babeli na Kutha na Aba, na Hamathi, na Sefarvaimu, akawaweka katika miji ya Samaria badala ya wana wa Israeli, waka umiliki Samaria wakakaa katika miji yake.”*

Je umesha wahi kuwa na Ujuzi Ufuatao?

Ulishawahi kuwekwa katika sehemu ambapo ni lazima usimame? Sehemu hii ya kusimamia isingekuwa maarufu sana.

Unachukuwa msimamo wako, ukifikiria wengine (au mwingine) akasimama na wewe. Lakini, kwa mshangao wako, ulikuwa peke yako. Ukasimamia kweli wewe pekee yako. Ilikuwa vigumu kwa sababu ya hofu.

Nina uakika kwamba wengi wetu wamekuwa katika hali kama hii.

Paulo alishawahi kukutana na swala kama hili:

2 Tim. 4:14-16, *“Iskanda mfua shaba alionyesha ubaya mwingi kwangu, Bwana atamlipa sawa na matendo yake. Nawe ujihadhari na huyo, kwa sababu, aliyapinga sana maneno yetu. Katika jawabu langu la kwanza hakuna mtu aliyesimama upande wangu, bali wote waliniacha, naomba wasihesabiwe hatia kwa jambo hilo.”*

Paulo anasema, “...hakuna mtu aliye simama upande wangu.....” alisimama peke yake! Inaitaji uvumilivu mwingi na ushujaa

1 Wakor. 15:58, “*Basi ndugu zangu wapendwa muimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwakuwa mwajua ya kuwa taabu yenu siyo bure katika Bwana.”*

Yesu pia alikuwa katika hali kama hii:

Alikamatwa na akajaribiwa pekee yake. Wanafunzi walimkataa. Petro pia akakimbia.

Bila kujali mazingira mtu wa Mungu hayuko peke yake.

Yesu aliahidi hii. Math. 28:18-20, *“Yesu akaja kwao, akasema nao, akawambia nimepewa mamlaka yote duniani na mbiguni. Basi, enendeni mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote*

niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari."

Sikiliza musita huu unao vutia katika Zaburi 56:9, *"Ndipo adui zangu watarudi nyuma yangu siku ile niitapo. Neno hili najua kuwa MUNGU yu upande wangu."* Umesikia hiyo?

Hebu tuchukue muda mfupi tujifunze kitu hapa ya ukweli huu:

Kwa nini Mungu yu upande wangu? Unajuwa ni kwa nini?

Hapa kuna baadhi ya sababu tunazojua kwamba Mungu yu upande wetu:

Kwa Sababu Biblia Inaifundisha

Mini ni chanzo cha tendo la kipeke la uumbaji kwa mkono wa Mungu.

Nimeumbwa kwa mfano wake. Mwanzo 1:26-27, *"Mungu akasema na tumfaanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu wakatawale samaki wa Baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi nyote pia, na kila chenye kutambaa kitaambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwana mume na mwana mke aliwaumba."*

Kwa viumbe vyote vya Mungu sisi ni wa kipekee, kwa sababu tuliumbwa kwa mfano wake.

Maandiko yanatupatia nguvu na faraja:

- 2 Petr. 1:3, *"Kwakuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vitupasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe."*
- Yuda 1:3, "*Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba muishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja."*

Kuna vitu vingi ambavyo Biblia imewahidi waaminifu:

- 1 Yoh. 4:4, *"Ninyi watoto wadogo mwatokana na Mungu nanyi mnawashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia."*

- Waef. 3:20, *"Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu."*

Kwa Sababu Niko Ndani Ya Kristo

Hakuna hukumu:

- Rumi. 8:1, "*Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu."*
- Waef. 1:7, "*Katika yeye huyo kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake."*

Sehemu hii ni ya ulinzi:

- 1 Yoh. 4:4, "*Ninyi watoto wadogo mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia."*

Kwa Sababu Ya Roho Mtakatifu

Tulipewa ili atusaidie:

- Matend. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*
- Matend. 5:32, *"Na sisi tu mashahidi wa mambo haya pamoja na Roho Mtakatifu, ambaye Mungu amewapa wote wamtiio."*

Anatudhibitishia uhakikisho wa Mungu:

- Waef. 1:13, *"Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu, tena mmekwisha kumwamini yeye na kutiwa mhuri wa Roho Yule wa ahadi aliye Mtakatifu."*
- Waru. 8:9, *"Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."*
- 1 Petr. 4:17, *"kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje?"*

Kwa Sababu Ya Maombi Yaliyojibiwa:

Hii ni chanzo kikubwa cha nguvu:

- Yako.1: 2-7, "*Ndugu zangu hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno. Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu awapaye wote, kwa ukarimu wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yoyote, maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama Yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana."*
- 1 Wathes. 5:17, *"Ombeni bila kukoma."*

Mungu anajibu maombi:

Anatupatia kile tunachokiitaji, sio tunacho kitaka. Imani ni ufunguo wa kufungulia ghal lake.

Matokeo Ya Mungu Kuwa Wa Kwangu

Uoga na mashaka vimeondoka:

2 Tim. 1:7, "*Wapenda kuwa waalimu wa sheria, ingawa hawayafahamu wasemayo wala mambo yale wayanenayo kwa uthabiti."*

Jaribu kuwa na ujasiri:

Kama Petro na Wakristo wa kwanza. Matend. 4:11-13, *"Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo. Basi walipoona ujasiri wa Petro na Yohana, na kuwajua ya kuwa ni watu wasio na elimu, wasio na maarifa, wakastaajabu, wakawatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu."*

Math. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akasema nao akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza, kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*

Usiwe na shaka kuhusu jinsi ambavyo watu wanaweza kukufikiria unapofanya kazi ya Bwana.

Mambo mengine yaliyo katika dunia hii ni machafu nay a kijinga, “ni wale tu wanao jiita kuwa wana akili sana” watawaamini.

Kuwa na ujasiri na utaushinda ulimwengu. Na Kristo unaweza kushinda kila mara.

- Wafil. 4:13, *“Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.”*
- Math. 5:8, “*Heri wenye moyo safi maana hao watamwona Mungu.”*

Hitimisho

Vipi kuhusu wewe? Je unaamini Mungu yu kwa ajili yako? Ameahidi hilo.

- Amelithibitisha. Math. 3:16, *“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanaye wa pekee ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.”*
- Waru. 8:31-39, *“Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwa upande wetu ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? Ni nani atakaye washitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye atakaye kufa; naam na zaidi ya hayo amefufuka katika wafu naye yuko katika mkono wa kuuma wa Mungu; tena ndiye anayetuombea. Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adh, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, Tume hesabiwa kama kondoo wa kuchinjwa. Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yasiyo juu, wala yasiyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.”*

Swali ni, “Wewe ni wa Mungu?” matendo yako na tabia yako inatoa jibu.

Yoshua 24:15, *“Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng’ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA.”*

Hiki ndiyo najua kwa hakika: Mungu ni wangu.